**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA**
*(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)*

*Unapojibu tafadhali taja;*
**Kumb. Na CDC/I.20/VOL 1/45**

**21 Julai, 2025**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA WAKUSANYA MAPATO VIJIJINI – NAFASI 114. REVENUE COLLECTORS**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba anawatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi ya kazi ya kukusanya mapato kama ifuatavyo:-

**1: SIFA ZA MUOMBAJI:**

i). Awe raia wa Tanzania;

ii). Awe na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea;

iii). Awe na elimu kuanzia Darasa la Saba na kuendelea;

iv). Awe ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba;

v). Awe na mdhamini atakaye mdhamini wakati wa kujaza mkataba (mke,mume,baba,mama au mtu yeyote mwenye mali isiyo hamishika kama vile shamba,nyumba n.k);

vi). Awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai au kuhukumiwa kifungo jela katika Mahakama yoyote;

vii) Awe tayari kufanya kazi katika eneo lolote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba;

viii) Yeyote aliyewahi kufanya kazi Halmashauri na kuisababishia hasara au upotevu wa mapato au kudaiwa na Halmashauri, **HARUHUSIWI KUOMBA KAZI HII;**

ix) Awe na namba ya **NIDA** itakayo tumika wakati wa usajili wa Mkusanya Mapato.

2. Masharti ya kuomba:

   a. Barua ya maombi ipitie kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji au Kata;
   b. Barua iambatane na picha ya muombaji na mdhamini wake zilizo pigwa siku za karibuni.

**2: MAJUKUMU YA MKUSANYA MAPATO:-**

i). Kukusanya mapato ya Halmashauri kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyopo katika eneo la Wilaya ya Chemba atakalopangiwa kufanya kazi kwa kutumia mashine ya Kielektroniki (POS);
ii). Kuwasilisha benki kupitia akaunti ya mapato ya Halmashauri makusanyo yote yaliyokusanywa kwa wakati katika siku za kazi au siku ya kwanza ya kazi ya wiki au baada ya sikukuu;
iii). Kutoa risiti za Mashine ya Kielektroniki (POS) kiasi sawa na fedha atakayopokea kutoka kwa mlipaji;
iv). Kutunza vifaa vya kukusanyia mapato (POS, Rejista) na Nyaraka za benki au Halmashauri zinazothibitisha uingizaji wa fedha benki;
v). Kufanya uhakiki kila siku wa makusanyo ya siku na taarifa ya mashine ya kukusanyia mapato na kuiwasilisha;
vi). Kuwasilisha Halmashauri mashine ya kukusanyia mapato (POS) kwa ajili ya Ukaguzi /uchunguzi na;
vii). Kufanya kazi nyingine zinazohusu mapato kwa kadri atakavyoelekezwa na Mwajiri.

**3: MUDA/ MASHARTI YA AJIRA.**

i). Ajira hii ni ya Mkataba wa miezi sita kuanzia mwezi Agosti 2025 hadi Januari 2026;
ii). Atakuwa chini ya uangalizi wa Mtendaji wa Kata na Kijiji husika na;
iii). Mkusanyaji ataongezewa mkataba kutokana na juhudi yake katika ukusanyaji wa mapato.

**4: MALIPO YA MKUSANYA MAPATO:-**

Malipo kwa kazi ya ukusanyaji mapato yatakuwa ni asilimia 5 (5%) ya mapato aliyokusanya na kuyawasilisha Benki kwa wakati

Maombi yatumwe ifikapo au kabla ya tarehe 28 Julai, 2025 kwa:
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S. L. P. 830,
**CHEMBA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 28 Julai, 2025 saa 9.30 mchana.

Hassan J. Mnyikah
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**CHEMBA.**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
CHEMBA